**KPSEA ALL STRANDS AND SUBSTRANDS TOPICALS**

# GRADE 6 TOPICAL QUESTIONS

# KISWAHILI

## VOLUME 1

*A Series of Revision Assessment Questions for each and every Strand & Sub-Strand prepared by top KPSEA KNAC Examiners.*

*Perhaps, The questions are meant to enhance the learners' content mastery and revision purposes as well*

REPUBLIC OF KENYA
MINISTRY OF EDUCATION

***For Marking Schemes Contact 0724333200 / 0768321553 or***

***Order online at:***

***www.kenyaeducators.co.ke***

**KENYA EDUCATORS CONSULTANCY**

# MASWALI YA MADA ZOTE GREDI YA SITA.

# KISWAHILI.

## KIFUNGU CHA 1: VIUNGO VYA MWILI VYA NDANI

**KISWAHILI**

**Shughuli za mwanafunzi**

Tunga sentensi tano zenye silabi 'ch' au 'sh'

a)

b)

c)

d)

e)

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Tambua maneno yenye silabi za sauti 'j' na 'nj'

1. Mbwa koko mwenye njaa alienda kwenye jaa lililokuwa limejaaa

2. Mama alitumia jungu kupikia njugu

3.Alipokuwa katika njozi aliota akitunukiwa jozi la viatu

Shughuli za mwanafunzi

Andika maneno manne yenye silabi ya sauti 'g' na 'ng'

a)

b)

c)

d)

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Tambua viungo vya ndani ya mwili zenye sifa zifuatazo

1. Kiungo cha mwill kinachotambua ladha ya chakula au kinywaji ni
2. Meno yanayoshikiliwa na nyama zinazoitwa
3. Kiungo kinachotumika kusafisha damu mwilinihuitwa
4. Kiungo kinachosafisha hewa huitwa
5. Damu hupitia wapi inapoenea mwilini

Tunga sentensi ukitumia misamiati ifuatayo

Moyo

Mbavu

Tumbo

Meno

Pafu

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Tambua kwa kupigia mstari vivumishi vya sifa katika sentensi hizi

- Mchezaji jasiri alituzwa.
- Nguo laini zimepingwa pasi.
- Mwanafunzi bora ametuzwa zawadi. - Matunda matamu yataliwa. .
- Nyuzi ndefu zitatumiwa kushona.

Tunga sentensi ukitumia vivumishi vya sifa vifuatavyo

Safi hodari

chafu

kubwa

refu

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Tunga sentensi ukitumia viashiria vifuatazo

a) haya

b)hapa

c)hii

d)huu

e)hili

**Shughuli za mwanafunzi**

Andika sentensi hizi kwa wingi

a) Redio yako

b) Kiatu chake

c) Nyumbani mwangu

d) Marashi yake

e) Mpira wako

Jaza kwa kutumia kimilikishi kifaacho

a) Jino .............. linauma ( lake, yake)

b) Kisu ............. ni kikali ( chake, zake)

c) Umoja ............. unafaa (yao, wao)

d) Sebuleni ............... pana wageni (petu , mwetu)

e) Nguo................ zinapendeza ( zao, yao)

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Taja majibu ya salamu zifuatazo

a) Makiwa

b) Tuonane kesho

c) Shikamoo _

d) Ndoto njema _

e) U mzima?

Jibu maswali yafuatayo

a) Habari za kushinda?

b) Alamsiki ni maamkuzi ya wakati upi?

c) Waambaje?

d) Wakati wa kumuaga mwenzako anapoenda kulala,utamwamkuaje?

e) Jibu la salamu “chewa’” ni

**Shughuli za mwanafunzi**

1.Tafuta maana ya maneno yafuatayo

a) jukumu

b) Mazingira

c) Maakulli

d) ghala

e) Kipepesi

f) ala

2. Soma maneno yafuatayo kisha uyapage jinsi yalivyo kwenye kamusi

Busara, ala, zana, bingwa,kipusa, chombo, dawati, rununu, fununu,farasi, simu

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Tunga sentensi ukitumia vivumishi vya idadi ifuatayo

a) watano

b) vichache

c) wengi

d) Hamsini

e) Milioni  mbili

Jaza pengo kwa kutumia maneno sahihi

a) viti

b) vipepeo

c) Wanafunzi

d) kitabu

e) Redio

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Tumia kirejeshi ~amba kujibu maswali haya

a) Vioo_____ vilivunjika ni vipya,

b) Nguo_______nitavaa Zimepigwa pasi

c) Uzi__________ulikatika ni wa mama,

d) Darasani________mna wanafunzi ni mkubwa.

e) Penseli____________ inaandika ni nzuri,

Tunga sentensi ukitumia virejeshi —amba vifuatavyo a) ambao

b) ambayo

C) ambako

d) ambazo

e) ambapo

**Shughuli za mwanafunzi**

Tumia kiwakilishi cha nafsi kinachofaa zaidi

a) ________tunajifunza kiswahili darasani (sisi, wao)

b) ___________alicheza vizuri uwanjani (mimi, yeye)

c) ___________mlisoma kwa bidii. (wale, nyinyi)

d) ___________nitachora vizuri ( sisi, mimi)

e) ___________wataimba nyimbo. (wale, nyinyi)

*Andika sentensi hizi kwa wingi*

a) Mimi ninasoma kwa bidii

b) Wewe huimba vuzuri

c) Ulifika saa ngapi?

d) Anasoma kitabu

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Jaza nafasi zifuatazo kwa kiwakilishi

a) _________vitatumiwa kesho. (hiki, hivi)

b) _____________watafundishwa wanafunzi (wale, huyu)

c) ____________zitanunuliwa kesho (zile, ile)

d) ___________pana wageni wengi (huko,hapo)

e) ____________kuna wanyama hatari (mle, kule)

**Shughuli za mwanafunzi**

Tumia kiwakilishi cha idadi sahihi kujibu maswali yafuatayo

a) __________watasafiri kesho ( saba, wasaba).

b) __________vitanunuliwa mwakani (nyingi,vingi)

c) ___________atachinjwa kesho (moja,mmoja)

d) ___________yatanunuliwa sokoni (matano, tano)

e) ___________zitaandaliwa nyumbani (nyingi, mengi)

Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vya idadi vifuatazo

a) Matatu

b) Mitano

c) Sita

d) Nyingi

e) Kadhaa

**Shughuli za mwanafunzi**

Tumia alama za uakifisho kujaza pengo

a) Je, utatutembelea lini_________

b) Jiwe lililumbikia majini chubwi_______

c) Kuna aina kadhaa za vivumishi

___________Vivumishi vya sifa, idadi, vimilikishi vya a-unganifu.

d) Wageni waling oa nanga asubuhi.

e) Lo _umemwona nyoka.

Tunga sentensi ukitumia alama zifuatazo za uakifishi kwa ufasaha

a) ?

b) !

c) .

d) :

e) .'

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Tunga sentensi ukitumia maneno haya ya heshima - a) Shehe

b) Rais

c) Mtawa

d) Hayati

e) Padre

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Andika wingi wa sentensi_hizi

a) Maskani yaliyojengwa yanapendeza

b) Maziwa yamemwangika yote

c) Makala yale yanavutia sana

d) Marashi yanayonukia

Taja wingi wa nomino hizi

a) Mafuta

b) Maarifa

c) Mate

d) Mamlaka

e) Mazingira

**Shughuli za mwanafunzi**

Kamilisha methali zifuatazo

a) Kinga kinga ndipo

b) Kidole kimoja

c) Mkataa wengi ni

d) Kofi hazili ila kwa

e) Chombo hakiendi ikiwa kila mmoja

**Shughuli za mwanafunzi**

Andika sentensi zifuatazo kwa wingi

a) Unga ulionunuliwa unamadhara

b) Uzuri wake ulimfanyia apendwe

c) Utajiri unadhirisha wengi

d) Usafi wa mazingira ni muhimu

e) Ukulima una manufaa nchini

Tunga sentensi ukitumia nomino zifuatazo

a) Moshi

b) Ushirikiano

c) Moto

d) utu

e) ulafi

**Shughuli za wanafunzi**

Andika sentensi hizi katika wingi

a) Chai iliyopikwa imemwangika

b) Mvua iliyonyesha ni ya masika

c) Baridi nyingi huleta madhara kwa mwili

d) Miwani ilianguka sakafuni ikavunjika

e) Damu iliyomwangika ni nyingi

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Tunga sentensi ukitumia nahau zifuatazo

a) Tia bidii

b) Piga jeki

c) Chapa Kazi

d) Kujifunga nira

e) Kuchanga bia

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Andika sentensi hizi kwa wingi

a) Uwanjani kunachezwa mpira

b) Kitandani pana blanketi

c) Mtaani kuna watu wengi

d) Msituni mna mnyama hatari

e) Shambani pana mazao mengi

Andika wingi wa maneno haya

a) Gari -

b) Dawatini

c) Mijini.

d) Tumboni -

e) Shambani

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Andika visawe vya maneno haya

a) Hasira

b) Cheo

c) Haya

d) Uzembe

e) Mvulana

**Shughuli za mwanafunzi**

Jaza jedwali hili

| | | |
|---|---|---|
| Tenda | Tendesha | tendeana |
| Imba | | |
| Cheza | | |
| Ruka | | |
| andika | | |

Nyambua vitenzi vifuatazo katika kauli ya kutendua

a) Kama

b) Chimba

c) Kosa.

d) Ziba

e) Panga

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Andika Vinyume vya maelezo haya

a) Mtoto mfupi amesimama

b) Njia pana itakarabatiwa

c) Mzigo mzito utabebwa

d) Kiti kichafu kitauzwa

e) Maswali rahisi yatajibiwa

Tunga sentensi ukitumia vivumishi hivi na kisha ukanushe

a) kali

b) Mwongo

c) Zuri

d) Refu

e) Zito .

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Jibu maswali kwa kutumia istiari sahihi

a)Rehema ni_________yeye ana maneno ming.

b) Wanajeshi ni ________wao hawatikisiki wala hawababaiki.

c) Kombo ni ________huwezi kumshika ukimfuata.

d)Wanafunzi ni _________wanaingia na kutoka darasani kila mara.

e) Nyumbani kwa shangazi ni _________kuna Mateso mengi.

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Eleza maana ya sentensi hizi

a) Ukisafiri mapema utafika

b) Angemwona mapema angempata

c) Ningalikula ningalishiba

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Kanusha sentensi zifuatazo

a) Wangepanda miti wangepata hewa safi.

b) Wasingaliambiwa wasingalijua.

c) Ukila vyakula bora utakuwa na afya njema.

d) Angesoma kwa bidii angefua dafu.

e) Ukimwona umwite.

**Shughuli kwa mwanafunzi**

Geuza sentensi hizi kwa hali ya

a) Kitabu chake kimeraruka (udogo)

b) Kichwa changu kimeoshwa ( ukubwa)

c) Jitanda lake limetandikwa ( wastani)

d) Kijitamba chake kimechafuka (wingi)

e)Kiatu chake kimetupwa (ukubwa)

Shughuli kwa mwanafunzi

Geuza sentensi zifuatazo katika kauli zifuatazo

a) Jiko lake la makaa limewaka (ukubwa).

b) Jani limeanguka ardhini (udogo).

c) Jijiwe lililotupwa ni kubwa (wastani)

d) Jijicho lake linauma sana (udogo)

e) Kijijiko chao kinawaka (wingi)

# KISWAHILI MITIHANI TATHMINI

## MTIHANI WA TATHMINI 1

**SEHEMU YA A ALAMA 20)**

*Soma maneno haya kwa sauti.*

Jaa

Doa

Choka

Goma

njaa

ndoa

shoka

ngoma

Taja vifaa vitano vya jikoni.

i *Andika maneno matano yenye sauti*

Th

na 'dh'

dh

**SEHEMU YA B**

**KUSOMA (ALAMA 10)**

*Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo*

Virusi vya korona ni kundi kubwa la virusi ambavyo kwa kawaida hupatika mionngoni mwa wanyama na vinaweza kusababisha kwa wanyama au binadamu. Maambukizi ya ugoniwa huu unashabihiana na ule wa mafua. Hadi wa sasa hakuna tiba au dawa maalum ya ugonjwa

Kunazo njia ainati zinazoweza ukongo huu wa virusi vya korona. Aidha ugonjwa huu huenezwa hasa kwa kutangamana na adinasi ambaye ameambukizwa na kuathirika, kugusa vifaa ambayo viliguswa au kupigwa chafya na mgonjwa aliye na virusi vya korona. Ni bayana kama mchana kuwa virusi hivi hupatikana kwenye chembechembe za mate au kamasi. Na vinaingia mwilini kwa kuguza au kupitia kwa kunywa, mapua au macho.

Uele huu una dalili zinazobadilika baina ya waathiriwa. Kwa wastani dalili hizi zinawezs

kuchua hadi siku ya na nne kuonekana. Idadi ya watu wanaoambukizwa huwa na dalili zisizo

na kuwapelekea wengi kupona bila kulazwa hospitalini.

1. Korona ni ugonjwa upi?

2. Taja njja mbili zinazoeneza korona.

3. Ugonjwa wa korona hupatikana katika chembechembe zipi?

4. Eleza dalili za ugonjwa wa korona.

5. Ugonjwa wa korona unashabihiana na ule wa

**SEHEMU YA C(ALAMA 20)**

**SARUFI**

1. *Andika vitanza ndimi vyenye silabı*

ch sh

d nd

g ng

Jaza pengo Taja majina ya vitu hivi



*Tunga sentensi ukitumia vivumishi zifuatazo*

A. Mzuri

B. Kichafu

C. Jeupe

D. Hodari

E. Ndefu

4. *Jibu maamkuzi na maagano*

a) Shikamoo

b) Alamsiki?

c) Hujambo

d) Safari njema

e) Umeshindaje

**SEHEMU YA D**

**KUANDIKA INSHA**

*UMUHIMU WA MISITU NCHINI*

## MTIHANI WA TATHMINI 2

**SEHEMU YA A (ALAMA 20)**

*Kusikiliza na kuzungumza*

*Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.*

a) Juma aliokota chuma hicho juma lililopita.

b) Msichana alichana nywle zake jana mchana.

c) Mjomba amenunua samani iliyoundwa zamani.

d) Shangazi alichoka baada ya kukata kuni kwa shoka.

e) Mkunjo ulikunjwa na adinasi wenye njaa kukicha.

2. Tunga sentensi yenye vivumishi vitano vya sifa

**SEHEMU YA B**

**KUSOMA**

*Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo*

Maana kamili ya UKIMWI ni ukosefu wa kinga mwilini. Ama kweli ugonjwa huu unasababishwa na virusi ambavyo huufanya mwili wa binadamu kukosa nguvu. Ugonjwa huu hauna tiba. Kwa njia mbalimbali zinazoeneza ugonjwa huu. Mathalan wajawazito huweza kuambukiza malaika mchanga anapojifungua au wanapowanyonyesha. Kutokuwa mwangalifu unapotumia vifaa vyenye ncha kali kama vile wembe ni njia moja wapo ya kusambaza uele huu.

Fauka ya hayo watu wanapojitosa katika anasa na kushiriki mapenzi kiholela bila shaka ukumbwa na uele huu. Njia nyingine ni kupitia tamaduni zilizopitwa na wakati kwa mfano upashaji tohara na ukeketaji.

Ama kwa hakika ugonjwa huu una dalili zake kwa mfano mja kukonda na kukondeana, upele mwilini, kukohoa mara kwa mara. Hali hii hupelekea mtu kuathirika kiafya kwa kudhoofika sana. Hatimaye kufariki. Aidha uchumi huzorota kwan taifa letu limewapoteza wajuzi wengi wenye tajriba katika nyanja mbalimbali. Bila kusahaau mayatima, wajane na umaskini katika familia nyingi.

1. Ukimwi ni

2. Virusi vya ukimwi huufanya mwili wa binadamu ukose

3. Taja njia mbili zilizotajwa wenye kifungu zinazoeneza UKIMWI

4. Taja dalili tatu za ugonjwa wa UKIMWI

5. Mayatima ni akina nani?

**SEHEMU YA C (ALAMA 20)**

1. *Taja sehemu hizi za mwili.*



*Tunga sentensi ukitumia vimilikishi vifuatavyo*.

a) Letu

b) Zao

c) Yangu

d) Wake

e) Chake

*3. Piga mstari kivumishi katika sentensizifuatazo*

a) Mwanafunzi bora atatuzwa zawadi.

b) Darasani pamejaa walimu.

c) Mama alipika chakula kidogo.

d) Kiatu hiki jeusi kitashonwa.

e) Jino lake linauma sana.

*4. Andika wingi wa sentensi zifuatazo*

a) Gari lingine linabeba abiria.

b) Kalamu yangu inaandika vizuri.

c) Mlima wenyewe una theluji.

d) Kuku ameangua kifaranga.

e) Maji yamemwangika sakafuni.

## SEHEMU YA D

## KUANDIKA INSHA

Andika insha ya kusisimua kuhusu "harusi iliyonipendeza"

## MTIHANI WA TATHMINI 3

**SEHEMU YA A**

*Kusikiliza na kuzungumza*

*1. Soma maneno haya kwa sauti*

Usalama wa trafiki barabarani unahusu njia na hatua zinazotumiwa kuzuia watumiaji wa barabara kuuawa au kujeruhiwa vibaya. Watumiaji wa kawaida wa barabara ni pamoja na watembezi wa miguu, waendesha baiskeli, wenye magari, abiria wa magari na wengine. Aidha kuna nia mbalimbali zinazosababisha ajali barabarani. Mathalan magari mabovu na kuukuu huweza kusababisha ajali kwa kukosa nguvu za kuhimili uzito.

Licha ya hayo njia mbovu zisizo na alama barabara ndio chanzo nyingine ya ajali.

Madereva hao wanahimizwa kutokuwa na upepetevu barabarani kwani wanapokosa umakini

wanaweza kusababisha ajali mwishowe maafa. Vilevile utumizi wa dawa za kulevya ndio suala

Iinaloibuka kuwa chanzo cha ajali barabarani, idara husika na jamii kwa nyumba yapaswa kupinga vikali kwa wanaotumia dawa za kuleyva

2. Andika salamu /maamkuzi matano na majibu yake

**SEHEMU YA B**

**KUSOMA (ALAMA 10)**

Siku moja

wakati wa jioni mvua ya rasharasha ilikuwa ikinyesha. Watu wengi walikuwa katika nyumba zao. Wengine walikuwa wakipata chajio zao. Familia zingine zilikuwa zikijikinga kutokana na baridi kwa kuota moto. Wachache sana walikuwa wakiwasili kutoka makazini. Ghafla bin vuu waja walisikia sauti kubwa ya kutishia. Punde si punde watu walitoka shoti hadi barasteni. Lori kubwa lilikuwa limeanguka baada ya kukosa mwelekeo na kubingirika.

Watu walimtoa dereva yule na kumsafirisha moja kwa moja hadi hospitali. Watu hawalifahamu kuwa chelewa chelewa utampata mwana si wako.

Watu wengine wenye tamaa ya fisi walipekua vijisanduku vilivyokuwa lorini na kutokomea pasipojulikana. Walipoyafungua vijisanduku hivyo walikuwa na nyemi kwani waliweza kupata maziwa.

Baada ya miezi miwili kuisha lori jingine lilianguka pale kijijini. Watu wale wabaya walifungua na kupata vijisanduku ndani ya lori. Waliyaiba na kuenda kuyaficha msituni. Usiku

walienda kuyafungua vijisanduku vile. Kelele na vilio vilisikika watu wale wakionekana wakitoka

shoti ungedhani walikuwa wameona mizuka. Kumbe lori lile lilikuwa la shirika la wanyama por

lilikuwa limebeba nyoka hatari haina ya chatu. Watu hao walitokomea wasie wakaonekana kwa

wiki mbili. Askari wa kuwalinda wanyama pori waliweza kuwaokoa nyoka. Ama kweli tamaa ni mbaya.

a) Ajali ilitokea wakati gani.

b) Baada ya waja kusikia sauti ya kuisha walifanya nini?

c) Watu wale walipofika barasteni walifanya nini?

d) Walipofungua vijisanduku kwa mara ya kwanza walipata nini?

e) Mbona watu walitoroka walipofika msituni?

**SEHEMU YA C**

**SARUFI (ALAMA 20)**

*1. Tumia kirejeshi (amba) panapostahili.*

a) Chai......amepika imeiva

b) Mguu..... uliumia ulitibiwa

c) Jino.........limeng'olewa limetupwa

d) Chakula...... .kimepikwa ni kitamu.

e) Kuku....... amechinjwa ni wangu.

*2. Kamilisha vitendawili vifuatavyo.*

a) Popoo mbili zavuka mto

b) Njoo umwone umpendaye

c) Achoki kubeba

d) Adui mpenzi

e) Bak bandika bak bandua

(moto, ardhi, kioo, macho, tembea)

*3. Jaza pengo kwa kutumia viwakilishi vya idadi.*

a) ___zimejengwa haraka. (wengi, nyingi, mingi)

B. ___amekiri makosa yake.(mmoja,moja)

C. _____ ametuzwa zawadi (wa kwanza, kwanza)

D. ____ vitanunuliwa kesho ( tano, vitano, matano)

E. ____ yatanunuliwa na baba (matatu, tatu)

*4. Kwa kutumia kamusi eleza maana ya*

A) Shehe

B) Kasisi

C) Mwadhini

D) Mheshimiwa

E) Mtawa

**KUANDIKA**

**INSHA**

Andika insha ya kusisimua ukurasa mmoja na nusu kuhusu kichwa kifuatacho

USAFI WA MAZINGIRA

## MTIHANI WA TATHMINI 4

**SEHEMU YA A (ALAMA 10)**

*Soma kifungu kifuatacho kina nafasi 1 - 10*

*Chagua jibu sahihi kujaza pengo*

Mkurupuko wa korona hadi kwa sasa umekuwa____ linalohitaji kuvaliwa njuga.

Kwani _____ vibaya nchi nyingi duniani na umesababisha hasara kubwa katika _____ mbalimbali za kiuchumi, zikiwemo usafiri, utalii, elimu, biashara na ukosefu wa kazi kwa mamilioni ya watu. Ueneaji wa _______ huu umeenea ulimwenguni kwa ____ mno.

Maelfu ya watu ____ kutokana na ugonjwa huu.

Nchi yetu ya kenya ni _____ mwa nchi ____ zimechukua hatua za kuepusha kuenea kwa ____ vya korona. Mfano kuwaweka ______ walioambukizwa kwa ajili ya matibabu.

(wameaga, kasi, ugonjwa, umeathiri, tatizo, sekta, miongoni, karantini, virus, ambazo)

**SEHEMU YA B**

**KUSOMA (ALAMA 10)**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata

Mayowe yalisikika kwa nyumba ya jirani sote tulipigwa na butwaa. Sauti hizo katu hazikuwa za kawaida kitongojini. Sote tulitazarnana uso kwa macho hapo sebuleni bila kunena lolote. Vyakula tulivyokuwa tukibugia yalisalia vivyo hivyo. Baba alitushauri tuwe watulivu ili tupate kunasa ukweli wa mambo.

Pindi tulisikia mwizi! Mwizi! Nafa! Jameni saidia. Bila shaka sauti hiyo tuliinasa barabara.

"sauti hii ni ya mzee fadhili" baba alisema kwa mshtuko.Bila kupunja hata sekunde baba alijitoma hadi nyumbani mwa kulala na kunyakua silaha yake tayari kukabiliana na wezi hao.

Wanakijiji waliweza kufika kwa boma la mzee Fadhili. Walishtuka walipompata mzee akiwa hali mahututi alikuwa akichungulia kaburi. Walimpa huduma ili kuyaokoa maisha yake,

Wanakijiji walianza mchakato wa kuwasaka wezi hao. Baba na wanakijiji wengine waliamua kuwasaka wezi hao katika msitu. Wezi wale walijaribu kutoroka lakini wapi. Wanakijiji walikuwa duma duma. Ama kweli siku za mwizi ni arobaini. Wezi wale walifumaniwa ghafla. Wanakijiji waliweza kuwakamata.

Wanakijiji walishirikiana kwani umoja ni nguvu. baba awasi kiambini usiku wa manane. Tulimshukuru Mungu kwa kumlinda.

1. Wakati mayowe yalisikika mwandishi walikuwa wapi wakifanya nini?

2. Ni nani aliyekuwa akivamiwa

3. Wanakijji walipofika kwa boma la Mzee Fadhili

4. Kwa nini wanakijiji waliwashika wezi hao

5. Baba aliwasili saa ngapi

**SEHEMU YA C**

**SARUFI (ALAMA 20)**

<u>*1. Tunga sentensi kwa kutumia maneno*</u>

yafuatayo.

a) Maziwa

b) Maji

c) Marashi

d) Mazingira

e) Mate

2. Kamilisha methali zifuatayo

a) Umoja ni nguvu

b) Jifya moja

c) Kinga na kinga

d) Mkono mmoja

e) Kidole kimoja

3. Tunga sentensi kwa kutumia maneno

haya.

a) Uji

b) Uhuru

c) Ujanja

d) Urafiki

e) Ugali

*4. Andika maneno haya kwa wingi,*

a) Mimi ninasoma kwa bidii

b) Wewe hutii bidii

c) Yeye hujitahidi kusoma

d) Ulifika saa ngapi

e) Anasoma gazeti

**KUANDIKA INSHA**

**Andika insha kuhusu**

MWALIMU WANGU

## MTIHANI WA TATHMINI 5

*Sehemu ya A alama 10)*

Mtu mmoja alikuwa na wana wawili. Mmoja alikuwa mtoto mwenye heshima. Yule mwingine alikuwa mtundu sana. Mtu huyo alijaribu kumrekebisha lakini hakufaulu. Hivyo basi alipotaka kumtuma mtu kitu angemchagua yule mwenye heshima. Alifahamu dhahiri shahiri kuwa angemtii.

Siku moja yule mtoto mnwenye heshima akaugua. Yule naye akapata jambo la maana sana hata hakuweza kumngojea apone akamtuma yule mtoto wake mtundu mji wa mbali kidogo na kwao.  Yule mtoto hakuelewa vyema maelezo ya njia kwa sababu alikuwa anachezacheza wala hatulii kusikiliza vema. Mwisho alishika njia aende kule alikotumwa na baba yake.

Njiani alisahaau maagizo. Alipofika njia panda hakujua aende upande wa kulia au kushoto. Akamwona mama mmoja ameketi kando anapumzika. Akamwuliza njia ya kufuata afike alikotumwa.

**Sehemu ya B**

**KUSOMA ALAMA**

Waswahil husema elimu ni taa gizani huzagaaa. Elimu ina manufaa anuwai ishabiku mchanga baharini. Elimu humwandaa mwanafunzi maisha mema baadaye.hakika mtaka cha

mnguni sharti ainame. Elimu vilevile humwezesha mtu kupata ajira ya kupendeza. Ili mwanafunzi au mtu yeyote afaulu maishani hana budi kuwa na hidhamu. Nidhamu ndio nguzo mojawapo inayomwelekeza mja maishani.

N lazima kama ibada mtu awe na heshima kwa wadogo na wakubwa. Haswa pia kuwa velelezo maishani Yakini heshima si utumwa. Taifa lolote linalopania kuboreka katika uchumi ni lazima raia wake kulipa kipaumbele suala la elimu. Hii itafikiwa iwapo kutakuwepo ushirikiano baina ya kila sekta. Ama kweli jifya moja haliinjiki chungu.

Elimu vilevile huimarisha mawasiliano kabambe baina ya watu. Mtu aliye na elimu aghalabu hutangamana vyema na wenzake haswa katika mawasiliano. Mtu anaweza kujieleza kwa ufasaha bila kuwa na changamoto nyingi. Mtu mwenye elimu katika jamii huonekana mtu mwenye hadhi. Jina lake hung'aa na kuwa jema.

Ili mtu yeyote aweze kuafikia malengo yake ya kielimu basi hana budi kuwa na bidii kama mchwa na mwenye maadili mema. Mja anastahili kujifunza maadili mema kwani atajaliwa baraka tele kutoka kwa wakuu wao. Asiwe mja mwenye tamaa bali avalie njuga la bidii. Ni bayana kama mchana kuwa bidii hulipa. Kando na hayo iwapo mwanafunzi angependa kufaulu katika masomo basi hana budi kuepuka

vitendo viovu maishani. Mfano ajiepushe na matumizi ya dawa za kulevya, marafiki wabaya au kuepuka ukaidi wa namna yoyote ile kwani wahenga walisema lila na fila havitangamani. lli malengo ya elimu yaweze kufanikishwa vyema ni jukumu la kila mmoja wetu katika jamii kuungana mikono ili kutekeleza yaliyo bora katika nyanja hii.

1 Ni nini maana va neno anuwai

2 Taja manufaa mawili va elimu katika kifungu.

3. Taja methali mbili za ushirikiano zilizotajwa kwenye kifungu.

4. Taja vitendo viwili ambavyo mwanafunzi ameimizwa kuviepuka.

5. lli malengo ya elimu kufanikiwa

**SEHEMU YA C**

**SARUFI (ALAMA 20)**

*1. Nomino hizi hupatikana katika ngeli gani*

a) Ujanja

b) Marashi

c) Sukari

d) Kipepeo

e) Cheo

2. Neno la heshima la kumwomba mtu akupishe njiani ni

*3. Kwa kutumia kamusi tambua maana ya maneno haya.*

a) Kambumbu

b) Gori

c) Hoki

d) Jugwe

e) Kibemasa

*4. Tumia vitenzi vilivyo kwenye mabano kujaza pengo.*

a) Nilim___ mama chakula ( leta, letea)

b) Mgeni ali___ na wenyeji (tembeza, tembezwa)

c) Dada amem ____ mtoto (laza, lalisha, lala)

d) Nyumba yetu ili____ (pambwa, pambika)

e) Chakula kime___ na mama (pikwa, pika, pikia)

*5. Tunga sentensi kwa kutumia alama zifuatazo*

a) ?

b) !

c) '

d).

**SEHEMU YA D- KUANDIKA**

**Andika insha ya kusisimua kuhusu.**

UMUHIMU WA KILIMO NCHINI

## MTIHANI WA TATHMINI YA 6

**SEHEMU YA A**

**Kusikiliza na kuzungumza (alama 10)**

*Mwalimu asome sentensi zifuatazo kwa sauti na umantiki*

a) Mwenzangu alinifaa sana aliponipa kabuti la kuvaa wakati wa baridi kali.

b) Baada ya kuvua nguo yangu nilifua nikaisuuza kisha nikaianika

c) Msusi alijifunga shuka kisha akaanza kumsuka nywele.

d) Ingawaje mwanafunzi yule alikuwa na shida ya kimaisha, alijitahidi na kushinda wenzake katika masomo.

e) Hamali alichoka sana baada ya kubeba mti aliokuwa ameukata kwa shoka.

**SEHEMU YA B**

**KUSOMA ALAMA (10)**

*Soma kifungu kifuatacho na ujibu maswali*

Nchi ya kenya ni kati ya nchi zilizotunukiwa rasilimali ainati. Kwanza ni zile mbuga ambazo wanyama mbalimbalı, mito ya kufurahisha, maziwa na mengineyo. Aidha zipo malighafi tele ambayo yanaboresha uchumi wa taifa letu. La hivi majuzi ni ugunduzi wa mafuta ghafi ambayo yanatarajiwa kuliimarisha nchi yetu na kuliweka katika orodha ya nchi zenye uchumi thabiti nchini. Si haya tu ambayo tunajivunia.

Katika miaka ya hivi karibuni nchi yetu imeweza kung'aa kimataifa. Katika nyanja ya michezo. Bila shaka wanamichezo hawa wamekuwa kipaumbele kuiletea sifa taifa letu la Kenya. Michezo ambayo imeweza kutia fora ni pamoja na riadha, kandanda, neti boli, jugwe, uogeleaji, raga na mingine mingi. Taifa letu limeweza kutambulika duniani kwa kuwa na wanariadha shupavu na tajika. Kando na hayo taifa letu limeweza kunufaika kutokana na pesa za kigeni.

Wachezaji hawa pia wamekuwa na la kutabasamu kwani imekuwa kitega uchumi na ajira kwa wengi, hivyo basi kuziwezesha familia zao kujikimu ipasavyo.

Ugatuzi vilevile umeleta maendelezo kabambe mashinani. Tangu kuwe na ugatuzi mambo mengi ya kimsingi yameweza kutokea. Kando na hapo awali sasa kuna mwanga wa maendeleo katika kila pembe ya nchi. Ugatuzi umeiwezesha kuimarika kwa miundo mingi Kwani barabara nyingi zimeweza

kutengenezwa huku zingine zikikarabatiwa. Wasafiri na wakulima waliokuwa wakilawama wengi wao kwa sasa wanatabasamu. Kwani usafiri umeweza kurahisishwa. Vilevile kumekuwa na maendeleo katika ujenzi wa hospitali, majengo ya umma na mahitaji mengine ya kimsingi ya wananchi. Wakenya wengi kwa sasa wanaweza kupata huduma kwa urahisi ikilinganishwa na enzi za hapo awali.

Japo baadhi ya habari zinazotoka huku nchini ni za kutamausha. Ama kweli hakuna masika yasiyokuwa na mbu. Visa vingi viovu huripotiwa kila kukicha mathalani visa vya ufisadi, ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana, ulaguzi wa mihadarati miongoni mwa vijana haswa wale waliona vyuoni Mauaji ya kiholela na mengine mengi. Serikali ikishirikiana na wananchi inafaa kuvalia uga maswala haya. Kwani kupitia kwa ushirikiano basi umoja na amani unaweza kuafikishwa kwani umoja ni nguvu. Viongozi nao wanapaswa kueneza amani miongonimwa raia ili kukuza utangamano wa taifa.

1. Taja aina mbili ya rasilimali zilizotajwa kwenye ufahamu.

2. Kwa kutumia kamusi tafuta maana yamaneno haya.

a) Malighafi

b) Rasilimali

c) Jikimu

d) Ugatuzi

3. Taja umuhimu mbili wa michezo katika taifa letu.

4. Taja manufaa ya ugatuzi yaliyotajwa katika ufahamu.

5. Taja baadhi ya visa vinavyotamausha nchini.

**SEHEMU YA C**

**SARUFI (ALAMA 20)**

*1. Taja visawe viwili vya majina haya.*

a) Mwizi

b) Hongo

c) Pesa

d) Nia

e) Maskini

*2. Jaza pengo kwa kutumia kiashiria kinachofaa zaidi.*

a) Kitabu___ kinapendeza sana

(hiki, hivyo)

b) Sebuleni___ mna wageni

(ile, kule, mle)

c) Miti____ ni mirefu sana

(huu, zile, hii)

d) Shambani____ pana wanyama hatari

(lile, pale)

e) Mjini ___ kumejengwa majumba makubwa

(mle, ule, kule)

*3. Andika sentensi zifuatazo katika wingi*

a) Simu ipi imeuzwa

b) Mti ambao umepandwa umenawiri

c) Kitabu kingine kimeletwa

d) Gari gani limeondoka

e) Kiroboto anauma

*4. Andika vinyume vya vivumishi hivi*

a) Mrefu

b) Safi

c) Kali

d) Rahisi

e) Pana

**SEHEMU YA D**

**INSHA**

Mwandikie mwalimu wako barua ukimweleza sababu zilizokufanya kutohudhuria vipindi vya masomo.

## MTIHANI WA TATHMINI 7

**SEHEMU YA A (ALAMA 10)**

*1. Soma maneno haya kwa sauti.*

Vua-fua

Jaa-njaa

Wasaa - saa

Pishi - bishi

Suka- shuka

Posa- poza

Baa - paa

Kula - kura

Mandari - mandhari

**SEHEMU YA B**

**Kusoma**

Mti ni mmea mkubwa wenye shina gumu. Unazo sehemu mbalimbali zikiwemo mizizi, matawi, shina, majani na matunda. Miti mingi iliyokusanyika pamoja huitwa msitu. Kuna Aina ainati. Kunayo iliyokua kwa nguvu za Mungu na mingine iliyopandwa na watu na kutunzwa na wenyewe.

Tangu jadi miti imekuwa yenye manufaa kochokocho. Watu wote huweza kufurahia manufaa yake. Ni dhahiri shahiri kuwa sote tunahitaji maji. Aghalabu maji haya hutokana na mvua ambayo chanzo chake ni miti. Mapafu ni ya kuvuta hewa, hewa ambayo huweza kutuweka hai. Hewa safi ambayo ni Oksijeni nayo hutokana na miti inapojitengenezea chakula.

Vilevile miti huvutia sana. Ni pombe la nchi na huboresha mandhari yake. Kwa minajili ya kuiona miti hii na kujiburudisha. Watalıı hufululiza nchini. Papo kwa papo kamba hukata jiwe hivyo basi pesa za kigeni huongezeka kila uchao. Mungu aliyekupa mastakimu yako aliwapa pia wanyama wa pori makazi yao kuwa mwituni. Hayo ndio makao yao. Unapozunguka katika nyumba zetu utagundua kuwa samani zilizomo zilitengenezwa kwa kutumia mbao. Bila miti basi hatungekuwa na malazi, nyumba, fanicha, kati ya vingine vingi.

Miti huwapa watu ajira. Wanakuza, kupalilia na kulinda misitu hupata riziki yao hapo.

Katika viwanda vya kutengeneza karatasi, nafasi za kupata ajira ni kabambe. Rasilimali za waja wengi hutokana na amali hi. Kwa mujibu wa hayo, tunaweza kusema kwamba miti ni uti wa mgongo wa taifa letu la kenya.

1. Taja aina moja ya miti iliyotajwa kwenye ufahamu.

2. Orodhesha sehemu tatu za mbili katika aya ya kwanza.

J. Je mo watu gani wanaonufaika na miti?

4. Eleza umuhimu tatu wa miti.

5. Fafanua maana ya maneno haya

Jadi

Shamiri

Mastakimu

6. Kabati, meza, viti, vitanda vyote ni

7. Kwa nini watalii huzuru nchini kulingana na ufahamu?

**SEHEMU YA C**

**SARUFI (ALAMA 20)**

*1. Kanusha sentensi zifuatazo*

a) Ningejitahidi ningeshinda.

b) Angesoma kwa bidii angepita mtihani.

c) Wangalipanda miti wangaliyatunza mazingira.

d) Mvua ingalinyesha miche ingalinyauka.

e) Ukisoma kwa bidii utafaulu.

*2. Jaza vitendawili vifuatavyo kwa majibu sahihi yatengue vitendawili vifuatavyo*

a) Wanashindana wakifuatana

b) Ninanye ng'ombe wangu ambaye hafanyi kazi nisipomshika mkono

c) Kwetu twalala tumesimama

d) Juu ya mlima kuna msitu mweusi

e) Bi mdogo lakini ajua kupika

*3. Andika vinyume vya sentensi zifuatazo*

a) Njia pana imetengenezwa.

b) Mama ameanika nguo.

c) Mbwa mkali hubweka.

d) Chungwa kubwa ni tamu.

e) Tuko mbali na mwanzo.

*4. Andika wingi wa sentensi hizi*

a) Gari jipya linapendeza.

b) Saa hii ni ya baba.

c) Mzee huyu ana busara sana.

d) Mjakazi huyu ni mtifu.

**SEHEMU YA D**

**KUANDIKA INSHA**

Andika insha ya kusisimua kuhusu

HASARA ZA KORONA

## MTIHANI TATHMINI 8

SEHEMU YA A(ALAMA 10)

*1. Soma kwa makini*

Jumamosi iliyopita ilikua ndiyo siku iliyotengewa sherehe ya kuzalıwa kwangu. Wageni walijumuika kwetu asubuhi na mapema. Nilizawadiwa vitu kadha wa kadha. Wakati wa hotuba ulipofika, nilisimama wima. Nikawaamkua watu wote waliohudhuria.

Kila mtu ana jukumu la kutekeleza katika jamii. mtu yeyote hafai kumndharau mwenzake Kila mmoja anakipawa ambacho anaweza kukuza na kujikimu yeye mwenyewe

2. Taja misamiati mitano katika kifungu hiki

a

Zama za kale watu wengi walisafiri masafa marefu kwa miguu. Ni wachache ambayo waliosfiri kwa kutumia punda na ngamia, leo hi usafiri umeimarika kiasi kwamba unaeza kusafiri umbali wa kilomita kadhaa kwa muda mchache ukitumia ndege.

Usafiri ambao unategemewa na wananchi wengi ni wa barabara.Hata hivyo, njia hii ya usafiri inakumbwa na matatizo belele. Nyingi za barabara zitumiwazo ni mbovu. Zimejaa mashimo ambayo hutatiza uendeshaji wa magari. Endapo dereva hawi makini ajali hutokea.

La kuchukiza na kukirihi ni msongamano wa magari katika miji mikuu.Hebu wazia, unatarajia kusafiri umbali wa kilomita tano kisha uchukue zaidi ya saa nzima, si heri upige milundi. Hali hukithiri mvua inyeshapo barabara hugeuka ziwa. Mitaro ya kupitisha maji huwa miembamba kiasi cha kutoweza kupitisha maji barabara. Wakati huu usafiri hukwama.

1 Zama za kale watu wachache walisafiri kwa kutumia

2. Ni usafiri upi unaotegemewa na wananchi wengi

3. Taja matatizo mawili yanayokumba usafiri wa barabarani

4. Eleza maana ya maneno haya

a. Kupiga milundi

b. Daladala

C. Ngwenje

5. Kwa nini usafiri hukwama wakatimwingine

6. Taja visawe vya maneno haya

a. Barabara

b. Daladala

7. Kwa nini madereva na utingo hupandisha nauli?

**SEHEMU YA C**

**SARUFI (ALAMA 20)**

*1. Andika katika hali ya udogo*

a. Mtoto huyo analia

b. Mwanamwali huyu ni mrembo

C. Mbuzi wa mama waliumia malishoni

d. Uso wake ni mweusi

e. Samaki huyu ni mtamu

*2. Andika katika hali ya ukubwa.*

a. Mbwa yule anabweka

b. Jina lake lilitajwa

C. Mwana huyu ni mtifu

d. Ukuta utajengwa

e. Ng'ombe yule anakula

*3. Tunga sentesi ukitumia viambishi vya hali ya masharti*

a. KI-

b. NGE-

C. NGALI-

d. KI-

e. NGE-

*4. Jaza pengo kwa kutumia istiara inayofaa*

a. Mzee huyo ni___ :mkali

b. Mwenzake ni ___: ana bidii.

c. Mjakazi huyo ni ____: anapenda kuongea sana.

d. Mwalimu wetu ni _____ :mrefu sana.

e. Nguo ya muhubiri ni ___ :ni nyeupe sana.

f. Binti huyu ni ____ :mrembo sana.

g. Kakake ni ____: ni mfupi sana.

h. Seremala huyo ni _____: ana ujanja wa kudanganya watu.

i. Mja yule ni ___ : ni mlafi na mwenye tamaa.

j. Maswali ya mtihani ni ____ ni rahisi sana.

**SEHEMU YA D**

**KUANDIKA INSHA**

Mwandikie rafiki yako barua ukimweleza jinsi unavyoendelea kimasomo

## MTIHANI WA TATHMINI 9

**Sehemu YA A ALAMA 10)**

*Jibu maaamkizi yafuatayo*

a) Hujambo?

b) Lala unono

c) Waambaje

d) Kwaheri

e) Alamsiki

f) Ugua polepole

g) Makiwa

h) Umeamkaje

i) Buriani

Mwakuliwa alikuwa mkaidi kama mkia wa nguruwe wanafunzi wen zake walimwonya dhidi ya kupitia njia ya mkato iliyopasua msitu wa Longo. Msitu huo ulikuwa na ndovu wengi wakubwa kama milima. Yeye aliwaambia kwamba zake zi mbali.

Siku moja alichukua baiskeli yake na kuanza safari. Nyuma ya baiskeli alifungua mkoba wake wa vitabu. Alipofika katikati ya msitu, dubwana lilitokezea kwa ghafla na kukinga njia. Mwakuliwa alipiga breki hima asimgonge kiumbe huyo lakini wapi!...

Alimgonga ndovu mguuni. Acha patokee hekaheka na patashika,

Ndovu aliidaka ile baiskeli na ule mkoba wake na kuivurumisha angani. Vitabu vilitoka mkobani na kupeperuka an gani mithili ya ndege weupe. Mwakuliwa alioonyoka na kuanguka chini.Nusura akanyagwe na dude hilo. Hapo alifungua pijo nambari miguu niponye. Ndovu aligeuka kumtafuta hasimu wake asimwone. Alienda tena ile baiskeli na kuitupa juu ya mti kwa hasira. Siku hiyo Mwakuliwa aliponea tundu la sindano. Tangu siku hiyo hataki hata kusikia kuwa kulikuwa na njia iliyopita katikati ya msitu. Ndipo alijua ni Heri tahadhari kabla ya hatari?

1) Marafiki wa mwakuliwa walimwonya dhidi ya kufanya nini?

2) Msitu huo hatari ulikuwa na nini?

3) Mwakuliwa alifanya nini alipoliona dubwana mbele yake?

4) Mwakuliwa alifanya nini baada ya kurushwa na ndovu?

D) "Ndovu wengi walikuwa wakubwa kama milima" kama iliyotumika katikaufahamu ni fani gani ya lugha?

6) Eleza maana ya maneno haya

a) Vurumisha

b) Hasimu

C) Ponea tundu la sindano

7) Mwakuliwa alijifunza nini?

**SEHEMU YA C**

**SARUFI (ALAMA-20)**

*Andika wingi wa nomino hizi*

1. Karatasi

2. Wembe

3. Uzi

4. Gari

5. Ua

*Tunga sentensi ukitumia misemo ifuatayo*

1. Kulaza damu -

2. Kata Kamba -

4. Shika sikio -

3. Uma kidole -

5. Mkono wazi -

6. Mkono birika -

7. Piga dua -

8. Kutia kapinu -

9. Kuwa maji na mafuta -

10. Shika usukani -

*Tumia kirejeshi'amba' kujazia mapengo*

1. Mtoto ___ alikuja mapema alisoma.

2.Njia ___ zinatumiwa kuwasiliana zinafaa.

3. Vyandarua ____ vilitumiwa vilisaidia sana.

4.Mahali ____ palikuwa na joka ni hapa.

5. Dhana ____ inafaa

**KUANDIKA**

**INSHA**

*Andika insha ya masimulizi kuhusu.*

Safari ILIYOPENDEZA

## MTIHANI WA TATHMINI 10

**SEHEMUYA A (ALAMA 10)**

*1 Andika visawe vya maneno yafuatayo.*

a) Tajiri

b) Familia

c) Barabara

d) Ugonjwa

e) Afya

*2.Andika maneno utakayosomewa na mwalimu au mwelekezi wako*

**SEHEMU YA B**

**KUSOMA SHAIRI**

Hebu nipe kalamu, natamani kuandika.

Nimtukuze karimu, Mola aliyesifika,

Alo daima dawamu, muumba alotukuka

Mola kaumba viumbe, katu hakuvibagua

Katu hakuvibagua, alipoumba viumnbe

Kwamba hiki ni murua, kile hakifai chembe,

Usawa kavipangia, kila moja kisigombe.

Vya kike na vya kiume, katu hakuvibagua.

Kiumbe dume na kike, katu hajavibagua

Kwamba moja kiteseke, kingine kufurahia,
Leo nalieleweke, hiyo siyo yake nia,
Mola kaumba viumbe, katu hakuvibagua.

Tamati ninaweza, nikihimiza umoja,
Tuungane ja mafiga, ni matatu silo moja,
Kwani chungu takibwaga, likiwepo jifya moja,
Mola kaumba viumbe, katu hakuvibagua.

1. Shairi hili ni la bahari gani?

2. Taja vina vya kati na vya mwisho vya

ubeti wa tatu.

3. Taja mshororo ambao ni mloto katika

ubeti wa pili.

4. Ubeti wa shairi hili una mizani mingapi?

5. Mwandishi anamsifu Mola kwa kuwa

6. Taja mleo wa ubeti wa nne.

7. Ubeti wa kwanza una mizani mingapi?

**SEHEMUYA C**

**SARUFI ALAMA 20)**

<u>*(a) Jibu maamkuzi yafuatayo*</u>

1. Hujambo

2. Alamsiki

3. Shikamoo

4. Buriani

6. Kwaheri

6. Waanbaje

7. Cheichei

8. Lala unono

9. Chewa

10.Hamjambo

(b) Jaza methali hizi

1. Mchagua jembe

2. Mgaa na upwa

3. Atafutaye

4. Anayejitahidi

5. Ukiona vyaelea

lc) Visawe

*Andika visa we vya maneno haya*

1. Msichana

2. Nyumbani

3. Ugonjwa

4. Rafiki

5. Mvulana

*(d) Orodhesha mapambo na mahali yanavaliwa*

1. Pete mkononi

2. Kipuli. Puani

3. Mkufu. Shingoni

4. Kipini. Sikio

5. Bangili. Kidole

**SEHEMU YA D**

**KUANDIKA: INSHA**

Endeleza insha ifuatayo:

Maji yana manufaa sana....